Pittsburgh Public Schools

Mwaka wa Masomo wa 2020-2022

# 6-12

# Sheria ya Maadili na Mwongozo wa Viwango vya Uvunjaji Sheria

Expect great things.

# Matendo ya Kiwango cha 1

**Matendo ya Kiwango cha 1 hayana vurugu.** Sio lazima Matendo ya kiwango cha 1 yawe na vitisho kwa afya, usalama au mali ya wengine. Uingiliaji na msaada unaofaa wa darasa na shule nzima hutumiwa kushughulikia matendo ya Kiwango cha 1. Wanafunzi hawapelekwi kwa msimamizi kwa ajili ya matendo ya kiwango cha 1 isipokuwa waendelee baada uingiliaji na usaidizi sahihi.

**101.A. Kuchelewa Kufika Shuleni:** Kufika baada ya muda wa kuanza uliochapishwa bila udhuru halali ulioandikwa.

**101.A. Kuchelewa Kufika Darasani:** Kufika baada ya muda wa kuanza darasa bila udhuru halali ulioandikwa.

**102. Utoro au Kukosa Darasa: Kutokuwepo bila ruhusa darasani au shuleni.**

**103. Mali ya Kibinafsi Isiyofaa: Umiliki na/au matumizi ya vitu ambavyo husababisha usumbufu wa masomo, uharibifu wa watu au mali, au vinginevyo kuingilia mchakato wa masomo.** Vitu visivyofaa vya mali ya kibinafsi vinaweza kujumuisha, lakini haijakomea tu kwa, kifaa cha kielektroniki, chakula kisichoruhusiwa, dawa ambayo haijasajiliwa na muuguzi wa shulechini ya Sera 229 - Matumizi ya Dawa, na Sera 229.1 - Umiliki/Matumizi ya Dawa za Dharura.

**104. Kusumbua, Kuchokoza, au Mchezo wenye Ghasia na Kelele: Kugusana kimwili au mawasiliano na mwanafunzi mwingine ambayo hufanywa kwa sababu zisizo za kielimu na inazuia elimu au usalama wa mazingira ya shule.**

**105. Lugha au Ishara Zisizofaa:** Maneno yaliyoandikwa au ya maneno au ishara zinazodhalilisha, kumtukana, au kuaibisha mtu au kikundi cha watu kupitia matumizi ya maneno au vitendo, pamoja na matumizi ya lugha au ishara chafu.

**106. Kutozingatia Kanuni za Mabasi Zilizochapishwa:** Ukiukaji wa sheria za maadili zilizochapishwa au zilizoandikwa za basi au shule; mifano: kutoketi kwenye kiti ulichopewa, kutofuata maombi ya wafanyakazi, kupanda au kushuka kwenye kituo cha basi kisichofaa.

**107. Kutozingatia Kanuni za Shule Zilizochapishwa:** Ukiukaji wa sheria na kanuni maalum za shule au darasa zilizochapishwa au zilizoandikwa; mifano inajumuisha, lakini, haijakomea tu kwa: kutafuna chingamu mara kwa mara, kuzungumza mara kwa maradarasani, kukimbia, kutupa vitu, na ukiukaji wa kanuni za mavazi.

**111. Umiliki wa Vifaa vya Kielektroniki au Mawasiliano:** Wanafunzi wanaweza kumiliki vifaa vya kielektroniki kama inaruhusiwa na sera ya Bodi na sheria za shule pekee. Kamati za Nidhamu zinazotegemea shule zinaweza kuweka vizuizi hivyo kwa njia ambayo inalingana na Sera ya Bodi 216 – Vifaa vya Kielektroniki. Wanafunzi na wazazi/walezi watapewa maelezo maalum kuhusu vizuizi vya vifaa vya kielektroniki mapema kabla ya kutekeleza kizuizi chochote.

Vizuizi vya vifaa vya kielektroniki havitatumika wakati mwanafunzi (1) ni mshiriki wa kampuni ya kujitolea ya moto, ambulensi au kikosi cha uokoaji; au (2) mwanafunzi ambaye anahitaji kifaa kama hicho kwa sababu ya hali ya kiafya ya mtu wa karibu wa familia. Wanafunzi wanaokiuka vizuizi vya vifaa vya kielektroniki wanaweza kuchukuliwa hatua za kinidhamu na kunyang'anywa kifaa.

**112. Kukatiza Darasa: Tabia** ya maneno au ya mwili ambayo huamuliwa na mwalimu wa darasa kuwa inakatiza masomo. Mifano inajumusha, lakini haijakomea tu kwa: kuzungumza mara kwa mara darasani au kwa zamu, kuwa wa sauti kubwa, kukimbia, kutupa vitu, kutofuata sheria za darasani.

**114. Matumizi Mabaya ya Kompyuta/Mitandao ya Kompyuta/Kifaa cha Kielektroniki: Mwanafunzi hatashiriki katika kitendo chochote kinachokiuka Sera ya Matumizi** na Usalama ya Wilaya, mwongozo wowote wa matumizi ya kompyuta ya shule au miongozo ya programu ya kifaa cha kompyuta, ikiwemo, lakini haijakomea tu kwa kufuata vitendo ambavyo haviwezi kusababisha tishio kwa afya, usalama, au mali ya wengine

A. Kutumia kompyuta, mitandao ya kompyuta, au vifaa vya kielektroniki wakati tabia kama hiyo hairuhusiwi.

B. Kupakia au kutumia kwa makusudi michezo, programu, faili au vifaa vingine vya kielektroniki visivyoidhinishwa kwenye vifaa vya Wilaya.

C. Kuiga mtumiaji mwingine, kutoa utambuzi, na majina bandia, ndani ya mifumo ya Wilaya.

D. Uundaji wa viungo kwa mitandao mingine ambayo maudhui au madhumuni yake yanaweza kukiuka Sera ya Matumizi na Usalama ya Mtandao ya Wilaya.

E. Mawasiliano ya kukera na uchochezi ambayo hayawezi kusababisha hatari yoyote kwa usalama Adabu inayofaa mtandaonii tafundishwa na kutekelezwa kabla ya kuendelea na nidhamu ya ukiukaji wa mwenendo wa kompyuta.

# Mifano ya Uingiliaji wa Mwongozo/ Mwendelezo wa Mbinu (Kiwango cha 1) (Mibadala ya Nidhamu Maalum)

- Matumizi ya Kanuni za Urekebishaji (kwa mfano, taarifa nzuri, maswali ya urekebishaji, vikundi, mikutano midogo isiyopangwa, n.k.)
- Rufaa kwa Mchakato wa Mifumo Mingi ya Misaada (MTSS)
- Rufaa kwa mipango ya utatuzi wa mizozo shuleni (kwa mfano, upatanishi wa wanarika)
- Mkutano wa mwanafunzi/mwalimu
- Mkutano wa mzazi au mlezi/ mwalimu
- Matarajio ya kufunza tena/mfano
- Mkutano wa mwanafunzi/msimamizi
- Uingiliaji kati wa kushauri wafanyakazi/mkutano wa mwongozo
- Kazi ya kutafakari iliyoandikwa
- Kuandaa, kukagua, au kurekebisha vifaa binafsi vya upangaji wa mwanafunzi (k.m, Mpango wa Usaidizi wa Tabia)
- Mabadiliko katika ratiba au darasa (na arifu ya mzazi/mlezi)
- Ushauri wa kibinafsi/kikundi
- Rufaa kwa Mpango wa Usaidizi wa Wanafunzi (SAP) kwa ajili ya uzuizi (k.m. vikundi vya mafundisho ya ustadi wa kijamii na kihisia kama udhibitiwa hasira, mbadala wa uchokozi, ustadi wa kupanga) na/au huduma za uingiliaji (k.v. huduma za ushauri wa afya ya kitabia)

- Mkutano/mpango wa kuboresha mahudhurio ya shule
- Mpango wa tabia ya mwanafunzi
- Rufaa kwa mpango wa ushauri
- Rufaa kwa Shirika la Jumuiya Lililoidhinishwa na Wilaya (CBO)
- Huduma ya jamii (kwa idhini ya mzazi/mlezi)
- Njia nyingine zinazofaa kwa nidhamu maalum (nidhamu maalum inajumuisha uzuiliwaji, Kuondoshwa kwa muda darani, Kuondoshwa kwa muda shuleni)

# Matendo ya Kiwango cha 2

**Matendo ya Kiwango cha 2 ni Mabaya Sana** na yanaweza kuwa tishio kwa afya, usalama, au mali ya mtu yeyote. Msimamizi hujulishwa wakati Matendo ya Kiwango cha 2 yanapotokea. Wanafunzi katika gredi ya 6-12 wanaweza kusimamishwa kwa ajili ya vitendo vya kiwango cha 2. Vitendo vilivyoorodheshwa katika italiki husababisha polisi wa shule kuarifiwa kulingana na Kanuni ya Shule Sehemu ya 1303-A (b) na 22 Pa. Kanuni Sehemu ya 10.22.

**202. Uharibifu wa Mali ya Shule: Kusababisha** au ujaribu kusababisha uharibifu wa mali ya shule.

**203. Kuharibu, au Kuvunja Mali ya Kibinafsi:** Kusababisha au kujaribu kusababisha uharibifu mkubwa kwa mali ya kibinafsi.

209. Wanafu nzi Kuwa Shuleni Bila Idhini Wakati wa Saa za Shule

**209.A. Kwenye Mazingira ya Shule:** Kuwepo kwenye mazingira ya shule wakati mwanafunzi haruhusiwi kuwapo (k.m., kwa sababu mwanafunzi amesimamishwa au ameombwa aondoke).
Kuwepo kwenye mazingira ya shule pamoja na mzazi/ mlezi kwa kusudi la kuhudhuria mkutano au kwa idhini ya mapema ya usimamizi wa shule haizingatiwi kama ukiukaji wa sheria hii.

**209B. 209.B. Kwenye Mali ya Kibinafsi au ya Umma:** Kuwepo kwenye mali ya kibinafsi au ya umma ambayo iko karibu na mali ya shule wakati wa saa maalum za shule. Wakati wa saa za shule, lazima wanafunzi wawe shuleni isipokuwa wana sababu iliyoidhinishwa ya kutokuwepo.

**210. Uvutaji sigara na Matumizi ya Tumbaku:** Kuvuta sigara, kutumia tumbaku au kifaa chochote cha kuvuta sigara cha kielektroniki katika majengo ya shule, mabasi ya shule, au kwenye mali yoyote inayomilikiwa, iliyokodishwa na au chini ya usimamizi wa shule.

**212.** Udanganyifu wa Kimasomo: Udanganyifu wa kimasomo utajumuisha, lakini haijakomea tu kwa, aina zote za udanganyifu,wizi wa maandishi, ufikiaji wa mitihani mapema,  kuwakilisha kazi ya mtu mwingine kama yao wenyewe, na matumizi yasiyoruhusiwa ya misaada wakati wa mitihani, miradi na kazi.

213. Unyanyasaji: Aina ya ubaguzi unaotegemea msingi wa mbari, rangi, umri, imani, dini, jinsia (pamoja na utambulisho wa jinsia au kujieleza kijinsia), mwelekeo wa kijinsia, ukoo, asili ya kitaifa, hali ya ndoa, ujauzito au ulemavu unaojumuisha tabia isiyofaa, au mwenendomwingine ambao unaweza kudhuru au kudhalilisha au kuingilia kati shule ya mtu au utendaji unaohusiana na shule wakati tabia hiyo ni mbaya sana, inaendelea, au imesambaa na mtu mwenye busara katika msimamo wa mlalamikaji atagundua kuwa inaleta mazingira ya kielimu ya kutisha, ya kuogofya aumabaya.

Ukiukaji maalum wa Unyanyasaji hufafanuliwa zaidi kama ifuatavyo:
**213.A. Unyanyasaji wa kingono:** Mwenendo kwa misingi ya jinsia ambayo haikubaliki na imedhamiriwa na mtu mwenye busara kuwa mbaya sana, unaosambaa na wa kukera kwa njia ambayo inamnyima mtu fursa sawa ya mpango wa Wilaya. Ubadilishaji wa kitu kimoja ili kupata kingine, unyanyasaji wa kingono, unaohitaji mtu kukubali mwenendo usiofaa wa kingono badala ya msaada, faida au huduma pia inajumuishwa kwenye sera ya Wilaya. Unyanyasaji wa kingono, unyanyasaji wa uchumba, unyanyasaji wa kinyumbani, na kuteka nyara, kama ilivyoainishwa katika sera ya Wilaya pia ni aina ya unyanyasaji wa kingono.

**213.B. Unyanyasaji wa kimbari/kikabila: Ubaguzi kwa misingi ya mbari, rangi, au asili ya kitaifa inajumuisha** ubaguzi kulingana na rangi halisi ya mtu au inayojulikana, rangi, asili ya kitaifa, kabila,au ukoo. Hii Inajumuisha ubaguzi kwa msingi wa nchi, eneo la ulimwengu, au mahali ambapo mtu au mababu wake walitoka; ustadi mdogo wa mtu wa Kiingereza au hali ya Mwanafunzi wa Kiingereza; au asili halisi au inayojulikana ya ukoo wa kushirikiwa au tabia ya kikabila, pamoja na ushirika katika dini ambalo linaweza kutambuliwa kuonyesha tabia kama hizo (kama vile Wahindu, Wayahudi, Waislamu, na Sikh).

**213.C. Unyanyasaji wa Kijinsia:** Inaweza kujumuisha vitendo vya vitisho vya maneno, visivyo vya maneno, au uchokozi au vitisho vya kimwili unaotegemea ubaguzi wa kijinsia. Kwa hivyo, unyanyasaji wa mwanafunzi kwa kushindwa kufuata dhana potofu za uanaume na uke ni ubaguzi wa kijinsia. Unyanyasaji unaotegemea jinsia unaweza kuongezeka kuwa ukiukaji wa sera ya Wilaya na/au Kichwa cha IX wakati mwenendo kama huo unakataza au kuzuia uwezo wa mwanafunzi kupata misaada ya kielimu, faida, huduma, au matibabu.

**213.D. Unyanyasaji wa Walemavu:** Vitisho au tabia ya dhuluma kwa mwanafunzi kulingana na ulemavu ambayo hutengeneza mazingira mabaya kwa kuingilia kati au kukataa mwanafunzi kushiriki katika au kupokea faida, huduma, au fursa katika mpango wa taasisi. Mwenendo wa unyanyasaji unaweza kujumuisha vitendo vya matusi na kutaja majina, pamoja na tabia isiyo ya maneno, kama vile taarifa za picha na maandishi, au mwenendo ambao unatishia kimwili, unaodhuru, auunadhalilisha.

**213.E. Aina zingine za Unyanyasaji:** Kitendo chochote ambacho kinakiuka Sera ya Kukataza Sera ya Uonevu/ Unyanyasaji ambayo haikidhi ufafanuzi wa unyanyasaji wa kingono, unyanyasaji wa rangi/kabila, unyanyasaji wa kijinsia, au unyanyasajiwa walemavu.

**214. Matumizi Mabaya ya Kompyuta/Mitandao ya Kompyuta/Kifaa cha Kielektroniki:** Mwanafunzi hatashiriki kwa makusudi katika kitendo chochote kinachokiuka Sera ya Matumizi na Usalama ya Mtandao ya Wilaya, miongozo yoyote ya matumizi ya kompyuta ya shule au miongozo ya programu ya kifaa cha kompyuta, ikiwemo lakini haijakomea tu kwa vifaa vifuatavyo na vya kibinafsi:

A. Barua za chuki, matamshi ya ubaguzi, pamoja na mawasiliano ya kukera na ya uchochezi ambayo yanasababisha hatari kwa usalama.

B. Kutumia kifaa chochote cha kielektroniki kuonyesha au kupata vifaa vya uchafu au ponografia.

C. Uhamisho wa lugha au picha zinazoonyesha ngono wazi, pamoja na picha zako mwenyewe.

D. Uharibifu, urekebishaji au matumizi mabaya ya maunzi ya mtandao, programu, au maelezo

E. Kuchukua video ya mapigano au kuchukua video ya mtu mahali ambapo ana matarajio ya kupata faragha.

F. Kuchapisha video za mwenendo usiofaa wa mwanafunzi kwenye tovuti ya mtandao wa kijamii inayoathiri jamii ya shule au watu binafsi ndani ya jamii ya shule kwa njia mbaya.

Adabu inayofaa mtandaoni itafundishwa na kutekelezwa kabla ya kuendelea na nidhamu ya ukiukaji wa mwenendo wa kompyuta.

**216. Kupigana:** Matumizi ya unyanyasaji wa kimwili kati ya wanafunzi wawili, ambapo haijulikani wazi baada ya uchunguzi kufanywa ni mwanafunzi yupi alikuwa mchokozi au mwanzilishi wa vita.

**217. Uonevu:** Uonevu inamaanisha kitendo cha kukusudia cha kielektroniki, maandishi, maneno au vitendo vya mwili au mfululizo wa vitendo vinavyoelekezwa kwa mwanafunzi au wanafunzi wengine, ambayo hufanyika katika mazingira ya shule, ambayo ni kali, inaendelea, au imesambaa na ina nia au athari ya:

1. Kuunda mazingira ya kutisha au uhasama ambayo yanazuia sana elimu ya mwanafunzi; au
2. Kumdhuru mwanafunzi Kimwili, kihisia, au kiakil; au
3. Kumfanya mwanafunzi awe na hofu isiyofaa ya kuumia kimwili au kihisa; au
4. Kumfanya mwanafunzi awe na hofu isiyofaa ya uharibifu au upotezaji wa mali ya kibinafsi

**217.B. Uonevu wa Mtandaoni:** U onevu unajumuisha uonevu mtandaoni na/au uonevu kupitia vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki ikiwemo, lakini haijakomea tu kwa, mitandao ya kijamii, barua pepe, ujumbe wa papo hapo, ujumbe wa maandishi, tweets (kupitia Twitter), blogu, kushiriki picha na video, vituo vya mazungumzo, dashibodi, au tovuti. Uonevu mtandaoni unaweza kujumuisha vitendo vinavyotokea nje ya shule ikiwa vigezo fulani vimetimizwa.

Makatazo kamili ya Sera ya Udhalimu/Unyanyasaji, taratibu za malalamiko na uchunguzi zimewekwa kwenye tovuti ya Wilaya katika www.pps.k12.pa.us/Page/481,  na katika kila majengo na darasa.

**218. Kudhalilisha:** Udhalilishaji hufanyika wakati mtu kwa makusudi, akijua, au bila kujali, kwa kusudi la kuanzisha, kukubali, au kumshirikisha mwanafunzi na shirika, au kwa kusudi la kuendelea au kuongeza ushirika au hadhi katika shirika, husababisha, analazimisha au kushurutisha mwanafunzi kufanya yoyote yafuatayo:

1. Kukiuka sheria ya shirikisho au serikali ya jinai.
2. Kutumia chakula chochote, kioevu, kioevu chenye kileo, madawa ya kulevya au kitu kingine chochote ambacho humuweka mwanafunzi kwenye hatariya kuumia kihisia au kimwili.
3. Kuvumilia ukatili wa asiliya akili, pamoja na shughuli zinazoathiri vibaya afya ya akili au hadhi yamtu huyo, kukosa usingizi,kutengwa kuwasiliana na jamii au mwenendo ambao unawezakusababisha aibu kubwa.
4. Kuvumilia ukatili wa asili ya kingono.
5. Kuvumilia shughuli nyingine yoyote ambayo hufanya uwezekano wa mwanafunzi kuumia kimwili.

Shughuli zilizo hapo juu zinachukuliwa kuwa za kudhalilisha bila kujali iwapo idhini ya mwanafunzi ilitafutwa au kupatikana..

**219.A. Mwenendo Mbaya na Utovu wa Adabu/Kubadilisha Matusi  (Mwanafunzi) (Isiyo ya Ukatili)*: Kuapa, kulaani, kufanya ishara chafu, au kutumialugha ya matusi kwa mwanafunzi mwingine.**

**219.B. Mwenendo Mbaya na Utovu wa Adabu/Kubadilisha Matusi (Mfanyakazi) (Isiyo ya Ukatili)*:** Kuapa, kulaani, kufanya ishara chafu, au kutumialugha ya matusi kwa mfanyakazi.

**220. Uchokozi/Mabishano ya Kimwili:** Matumizi ya vurugu na mwanafunzi kwa mtu mwingine wakati hakuna jeraha kubwa kama inavyoamuliwa na msimamizi wa shule, lakini kuna mchokozi au mwanzilishi wa uchokozi wa kimwili.

**221. Vitisho vya kigaidi (visivyo vya vurugu)*:**Tishio limewasilishwa moja kwa mojaau kwa njia isiyo ya moja kwa moja ili kufanya uhalifu wowote wa vurugu kwania ya kumtisha mwingine; kusababisha uhamaji kwenye jengo, mahali pa kusanyiko au kituo cha usafirishaji wa umma; au vinginevyo kusababisha usumbufu mkubwa wa umma, au kusababisha hofu au usumbufu mkubwa wa umma bila kujalihatariya kusababisha hofu au usumbufu kama huo.

**222. Tabia Isiyofaa ya Kingono :** Kuonyesha au kugusa sehemu za siri, kifua, au matako ya mtu, au sehemu za siri za mtu mwingine. Inaweza pia kujumuisha kujihusishangono, ngono ya mdomoni,au kuiga vitendo vyangono kwenye uwanja wa shule.

**223. Kuchochea usumbufu au Ghasia Nyingi: Kusababisha** usumbufu mkubwa au mapigano kati ya kikundi cha watu, na kusababisha wafanyakazi wengi wa shule kuhusika kutuliza usumbufu.

**225. Vitisho:** Tishio la kufanya vurugu. Vitisho katika kiwango hiki vina hatari ndogo kwa mwathiriwa nausalama wa umma.Tishio sio dhahiri na si la moja kwa moja; maelezo yaliyo ndani ya tishio hayalingani, yasiyowezekana au hayana maelezo ya kina; tishio halina uhalisia; na maudhui kwenye tishio yanaonyesha kuwa mtu huyo hawezi kutekeleza. Vitisho vinaweza kufanywa kwa maneno, kwa maandishi, au kwa ishara.

**226.A. Wizi wa Mali ya Shule:** Mwanafunzi hatashiriki au kujaribu kushiriki katika wizi wa mali ya shule.

**226. Wizi wa Mali ya Kibinafsi ya Mwanafunzi: Mwanafunzi** hataiba au kujaribu kuiba kutoka kwa mwanafunzi au kuiba mali ya kibinafsi.

# Mifano ya Uingiliaji wa Mwongozo/ Mwendelezo wa Mbinu (Kiwango cha 2)

- Matumizi ya Kanuni za Urekebishaji (k.v taarifa nzuri, maswali ya urejesho, vikundi, mikutano midogo isiyopangwa, mkutano rasmi wa urejesho, n.k.)
- Rufaa kwa Mchakato wa Mifumo Mingi ya Misaada (MTSS)
- Rufaa kwa mipango ya utatuzi wa mizozo shuleni (kwa mfano, upatanishi wa wanarika)
- Mkutano wa mwanafunzi/mwalimu
- Mkutano wa mzazi au mlezi/ mwalimu
- Matarajio ya kufunza tena/mfano
- Mkutano wa mwanafunzi/msimamizi

• Uingiliaji kati wa kushauri wafanyakazi/mkutano wa mwongozo

• Kazi ya kutafakari iliyoandikwa

• Kuandaa, kukagua, au kurekebisha vifaa binafsi vya upangaji wa mwanafunzi (k.m, Mpango wa Usaidizi waTabia)

• Mabadiliko katika ratiba au darasa(na arifu ya mzazi/mlezi)

• Ushauri wa kibinafsi/kikundi

• Rufaa kwa Mpango wa Usaidizi wa Wanafunzi (SAP) kwa ajili ya uzuizi (k.m. vikundi vya mafundisho ya ustadi wa kijamii na kihisia kama udhibiti wa hasira, mbadala wa uchokozi, ustadi wa kupanga) na/au huduma za uingiliaji (k.v.huduma za ushauri wa afya ya kitabia)

• Mpango wa tabia ya mwanafunzi

• Rufaa kwa mpango wa ushauri

• Rufaa kwa Shirika la Jumuiya Lililoidhinishwa na Wilaya (CBO)

• Huduma ya jumuiya (kwa idhiniya mzazi)

• Njia nyingine zinazofaa kwa nidhamu maalum (nidhamu maalum inajumuisha uzuiliwaji, Kuondoshwa kwa muda darasani, Kuondoshwa kwa muda shuleni)

# Mifano ya Hatua za Kinidhamu Zilizopendekezwa Baada ya au Kuongezea kwa Mbinu za Mwongozo Zilizotumika (Kiwango cha 2)

• **Zuio:** Kuwekwa katika eneo maalum la shule nje ya saa za shule (k.m, kabla ya shule, baada ya shule, au siku isiyo ya shule)

• **Kuondoshwa kwa muda shuleni:** Kutengwa kutoka kwa madarasa na kuwekwa katika nafasi maalum ya kujifunza. Mpango huu unaweza kupewa jina zaidi ya "Kuondoshwa kwa muda shuleni" ulio maalum kwa mfumo wa PBIS wa kila shule. Kuondoshwa kwa muda shuleni kunaweza kutekelezwa tu kulingana na mwongozo wa usimamizi uliotolewa na Msimamizi na Msimamizi Msaidizi wa Huduma za Usaidizi wa Wanafunzi.

• Mibadala mingine inayofaa ya kusimamishwa nje ya shule

• Kusimamishwa kwenda safari za nje, mikusanyiko, au faida nyingine maalum

• Kutolewa kwa shughuli za nje ya shule

• Faida za usafirishaji kusimamishwa

• Kutolewa kwa matukio maalum au mazoezi ya ukuzaji

• Kuondoshwa kwa muda shuleni (siku 1-3)

# Matendo ya Kiwango cha 3

**Vitendo vya Kiwango cha 3 ni vya hali mbaya** na yanaweza kuwa tishio kwa afya, usalama, au mali ya mtu yeyote. Msimamizi hujulishwa wakati kitendo cha Kiwango cha 2 kinapotokea. Wanafunzi wanaweza kufukuzwa kwa ajili ya hatua yoyote ya Kiwango cha 3. Vitendo vilivyoorodheshwa katika italiki husababisha polisi wa shule kuarifiwa kulingana na Kanuni ya Shule Sehemu ya 1303-A (b) na22 Pa. Kanuni Sehemu ya 10.22.

**302.A. Uharibifu wa Mali ya Shule: Mwanafunzi hatasababisha** au kujaribu kusababisha uharibifu wa mali ya shule, au kuiba au kujaribu kuiba mali ya shule. Uharibifu, kuvunja, au wizi katika kiwango hiki unazidi dola mia moja ($100).

**302.B. Uharibifu wa Mali ya Kibinafsi: Mwanafunzi hatasababisha au** kujaribu kusababisha kwa makusudi uharibifu mkubwa wa mali ya kibinafsi, au kuiba au kujaribu kuiba mali ya kibinafsi. Mali ya kibinafsi yenye thamani haipaswi kuletwa shuleni.  Uharibifu au wizi katika kiwango hiki cha unazidi dola mia moja ($100).

**307. Madawa ya kulevya pamoja na makosa madogo ya Bangi, Vifaa, na Pombe:** Mwanafunzi hatamiliki, kutumia, kusambaza, au kuwa chini ya ushawishi wa kilevi chochote cha aina yoyote. Hata hivyo, katika juhudi za kupunguza nidhamu maalum, majibu nzuri ya kushughulikia dawa za kulevya kulingana na ukali wa kosa imeainishwa kulingana na vikundi vya makosa ya dawa kwenye ukurasa wa 15. Ukiukaji wa Kanuni ya 307 inajumuisha makosa ya mara ya kwanz ya bangi chini ya gramu 5, pombe, na umiliki wa vifaa unaotokea katika mwaka mmoja wa shule. Tafadhali kumbuka kuwa matumizi ya agizo la dawa lililoidhinishwa kutoka kwa daktari aliyesajiliwa kwa mwanafunzi ambaye ameagizwa haitazingatiwa kama ukiukaji wa sheria hii, lakini inaweza kuwa ukiukaji wa sera ya Wilaya ya Matumizi ya Dawa. Kukosa kufuata Sera ya Matumizi ya Dawa pia kunaweza kusababisha nidhamu ya shule.

**313. Unyanyasaji:** Aina ya ubaguzi unaotegemea msingi wa mbari, rangi, umri, imani, dini, jinsia (pamoja na utambulisho wa jinsia au kujieleza kijinsia), mwelekeo wa kijinsia, ukoo, asili ya kitaifa, hali ya ndoa, ujauzito au ulemavu unaojumuisha tabia isiyofaa, au mwenendo mwingine ambao unaweza kudhuru au kudhalilisha au kuingilia kati shule ya mtu au utendaji unaohusiana na shule wakati tabia hiyo ni mbayasana, inaendelea, au imesambaa na mtu mwenye busara katika msimamo wa mlalamikaji atagundua kuwa inaleta mazingira ya kielimu ya kutisha, ya kuogofya au mabaya.

**Ukiukaji maalum wa Unyanyasaji hufafanuliwa zaidi kama ifuatavyo:**

**313.A. Unyanyasaji wa kingono:** Mwenendo kwa misingi ya jinsia ambayo haikubaliki na imedhamiriwa na mtu mwenye busara kuwakalisana, unaosambaa na ya kukera kwa njia ambayo inamnyima mtu fursa sawa ya mpango wa Wilaya. Quid proo quo unyanyasaji wa kingono, unaohitaji mtu kukubali mwenendo usiofaa wa kingono badala ya msaada, faida au huduma pia inajumuishwa kwenye sera ya Wilaya. Unyanyasaji wa kingono, unyanyasaji wa uchumba, unyanyasaji wa kinyumbani, na kuteka nyara, kama ilivyoainishwa katika sera ya Wilaya pia ni aina ya unyanyasaji wa kingono.

**313.B. Unyanyasaji wa kimbari/kikabila:** Ubaguzi kwa misingi ya mbari, rangi, au asili ya kitaifa inajumuisha ubaguzi kulingana na rangi halisi ya mtu au inayojulikana, rangi, asili ya kitaifa, kabila, au ukoo. Hii Inajumuisha ubaguzi kwa msingi wa nchi, eneo la ulimwengu, au mahali ambapo mtu au mababu wake walitoka; ustadi mdogo wa mtu wa Kiingereza au hali ya Mwanafunzi wa Kiingereza; au asili halisi au inayojulikana ya ukoo wa kushirikiwa au tabia ya kikabila, pamoja na ushirika katika dini ambalo linaweza kutambuliwa kuonyesha tabia kama hizo (kama vile Wahindu, Wayahudi, Waislamu, na Sikh).

**213.C. Unyanyasaji wa Kijinsia:** Inaweza kujumuisha vitendo vya vitisho vya maneno, visivyo vya maneno, au uchokozi au vitisho vya kimwili unaotegemea ubaguzi wa kijinsia. Kwa hivyo, unyanyasaji wa mwanafunzi kwa kushindwa kufuata dhana potofu za uanaume na

uke ni ubaguzi wa kijinsia. Unyanyasaji unaotegemea jinsi aunaweza kuongezeka kuwa ukiukaji wa sera ya Wilaya na/au Kichwa cha IX wakati mwenendo kama huo unakataza au kuzuia uwezo wa mwanafunzi kupata misaada ya kielimu, faida, huduma, au matibabu.

**313.D. Unyanyasaji wa Walemavu:** Vitisho au tabia ya dhuluma kwa mwanafunzi kulingana na ulemavu ambayo hutengeneza mazingira mabaya kwa kuingilia kati au kukataa mwanafunzi kushiriki katika au kupokea faida, huduma, au fursa katika mpango wa taasisi. Mwenendo wa unyanyasaji unaweza kujumuisha vitendo vya matusi na kutaja majina, pamoja na tabia isiyo ya maneno, kama vile taarifa za picha na maandishi, au mwenendo ambao unatishia kimwili, unaodhuru, auunadhalilisha.

**213.E. Aina Nyingine za Unyanyasaji:** Kitendo chochote ambacho kinakiuka Sera ya Kukataza Sera ya Uonevu/ Unyanyasaji ambayo haikidhi ufafanuzi wa unyanyasaji wa kingono, unyanyasaji wa rangi/kabila, unyanyasaji wa kijinsia, au unyanyasaji wa walemavu.

**114. Matumizi Mabaya ya Kompyuta/Mitandao ya Kompyuta/Kifaa cha Kielektroniki:** Mwanafunzi hatashiriki katika kitendo chochote kinachokiuka sera ya Matumizi na Usalama ya Wilaya, mwongozo wowote wa matumizi ya kompyuta ya shule au miongozo ya programu ya kifaa cha kompyuta, ikiwemo, lakini haijakomea tu kwa, kufuata vitendo ambavyo haviwezi kusababisha tishio kwa afya, usalama, au mali ya wengine:

A. Barua ya chuki, matamshi ya kibaguzi, pamoja na mawasiliano ya kukera na ya uchochezi ambayo yanasababisha hatari kwa usalama

B. Kutumia kifaa chochote cha kielektroniki kuonyesha au kupata vifaa vya uchafu au ponografia.

C. Uhamisho wa lugha au picha dhahiri za kingono, pamoja na picha zako mwenyewe

D. Uharibifu, mabadiliko au matumizi mabaya ya vifaa vya mtandao, programu, au maelezo

E. Kuchukua video ya mapigano au kuchukua video ya mtu mahali ambapo ana matarajio ya kupata faragha.

F. Kuchapisha video za mwenendo usiofaa wa mwanafunzi kwenye tovuti ya mtandao wa kijamii inayoathiri jamii ya shule au watu binafsi ndani ya jamii ya shule kwa njia mbaya.

Adabu inayofaa mtandaoni itafundishwa na kutekelezwa kabla ya kuendelea na nidhamu ya ukiukaji wa mwenendo wa kompyuta.

**317. Uonevu:** Uonevu inamaanisha kitendo cha kukusudia cha kielektroniki, maandishi, maneno au vitendo vya mwili au mfululizo wa vitendo vinavyo elekezwa kwa mwanafunzi au wanafunzi wengine, ambayo hufanyika katika mazingira ya shule, ambayo ni kali, inaendelea, au imesambaa na ina nia au athari ya:

1. Kuunda mazingiraya kutisha au uhasama ambayo yanazuia sana elimu ya mwanafunzi; au

2. Kumdhuru mwanafunzi Kimwili, kihisia, au kiakil; au

3. Kumfanya mwanafunzi awe na hofu isiyofaa ya kuumia kimwili au kihisa; au

4. Kumfanya mwanafunzi awe na hofu isiyofaa ya uharibifu au upotezaji wa mali ya kibinafsi

**317.B. Uonevu wa Mtandaoni: Uonevu** unajumuisha uonevu mtandaoni na/au uonevu kupitia vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki ikiwemo, lakini haijakomea tu kwa, mitandao ya kijamii, barua pepe, ujumbe wa papo hapo, ujumbe wa maandishi, tweets (kupitia Twitter), blogu, kushiriki picha na video, vituo vya mazungumzo, dashibodi, au tovuti.

Makatazo kamili ya Sera ya Udhalimu/Unyanyasaji, taratibu za malalamiko na uchunguzi zimewekwa kwenye tovuti ya Wilaya katika www.pps.k12.pa.us/Page/481,  na katika kila majengo na darasa.

**218. Kudhalilisha:** Udhalilishaji hufanyika wakati mtu kwa makusudi, akijua, au bila kujali, kwa kusudi la kuanzisha, kukubali, au kumshirikisha mwanafunzi na shirika, au kwa kusudi la kuendelea au kuongeza ushirika au hadhi katika shirika, husababisha, analazimisha au kushurutisha mwanafunzi kufanya yoyote yafuatayo:

1. Kukiuka sheria ya shirikisho au serikali ya jinai.

2.Kutumia chakula chochote, kioevu, kioevu chenye kileo, madawa ya kulevya au kitu kingine chochote ambacho humuweka mwanafunzi kwenye hatariya kuumia kihisia au kimwili.

3.Kuvumilia ukatili wa asili ya akili, pamoja na shughuli zinazoathiri vibaya afya ya akili au hadhi ya  mtu huyo, kukosa usingizi, kutengwa kuwasiliana na jamii au mwenendo ambao unaweza kusababisha aibuk ubwa.

4.Kuvumilia ukatili wa asili ya kingono.

5. Kuvumilia shughuli nyingine yoyote ambayo hufanya uwezekano wa mwanafunzi kuumia kimwili.

Shughuli zozote zilizoelezwa hapo juu zinachukuliwa kuwa za kudhalilisha bila kujali iwapo idhini ya mwanafunzi ilitafutwa au kupatikana.

**321. Vitisho vya kigaidi:** Tishio limewasilishwa moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja ili kufanya uhalifu wowote wa vurugu kwa nia ya kumtisha mwingine; kusababisha uhamaji kwenye jengo, mahali pa kusanyiko au kituo cha usafirishaji wa umma; au vinginevyo kusababisha usumbufu mkubwa wa umma, au kusababisha hofu au usumbufu mkubwa wa umma bila kujalihatariya kusababisha hofu au usumbufu kama huo.

**322. Tendo a kujamiiana/Utovu wa nidhamu:**Utovuwanidhamuwakingono katikakiwangohikichaukiukajiunajumuishakushirikitendolakujamiana, ngono ya kinywa, au kuiga vitendo vya ngono kwenye uwanja wa shule.

**223. Kuchochea usumbufu au Ghasia Nyingi: Kusababisha** usumbufu mkubwa au mapigano kati ya kikundi cha watu, na kusababisha wafanyakazi wengi wa shule kuhusika kutuliza usumbufu.

**326.A. Wizi, wa Mali ya Shule: Mwanafunzi hataiba** au kujaribu kuiba mali ya  .Wizi katika kiwango hiki na inazidi $100.

**326.B. Wizi wa Mwanafunzi au Mali ya Kibinafsi: Mwanafunzi hataiba** au kujaribu kuiba kutoka kwa mwanafunzi au kuiba mali ya kibinafsi. Wizi katika kiwango hiki inazidi $100.

# Mifano ya Uingiliaji wa Mwongozo/ Mwendelezo wa Mbinu (Kiwango cha 2)

• Matumizi ya Kanuni za Urekebishaji (k.v taarifa nzuri, maswali ya urejesho, vikundi, mikutano midogo isiyopangwa, mkutano rasmi wa urejesho, n.k.)

• Rufaa kwa Mchakato wa Mifumo Mingi ya Misaada(MTSS)

• Rufaa kwa mipango ya utatuzi wa mizozo shuleni (kwa mfano, upatanishi wa wanarika)

• Mkutano wa mwanafunzi/mwalimu

• Mkutano wa mzazi au mlezi/mwalimu

• Matarajio ya kufunza tena/mfano

• Mkutano wa mwanafunzi/msimamizi

• Uingiliaji kati wa kushauri wafanyakazi/mkutano wa mwongozo

• Kazi ya kutafakari iliyoandikwa

• Kuandaa, kukagua, au kurekebisha vifaa binafsi vya upangaji wa mwanafunzi (k.m, Mpango wa Usaidizi wa tabia)

• Mabadiliko katika ratiba au darasa (na arifu ya mzazi/mlezi)

• Ushauri wa kibinafsi/kikundi

• Rufaa kwa Mpango wa Usaidizi wa Wanafunzi (SAP) kwa ajili ya uzuizi (k.m. vikundi vya mafundisho ya ustadi wa kijamii na kihisia kama udhibiti wa hasira, mbadala wa uchokozi, ustadi wa kupanga) na/au huduma za uingiliaji (k.v. huduma za ushauri wa afya ya kitabia)

• Mpango wa tabia ya mwanafunzi

• Rufaa kwa mpango wa ushauri

• Rufaa kwa Shirika la Jumuiya Lililoidhinishwa na Wilaya (CBO)

• Huduma ya jumuiya (kwa idhiniya mzazi)

• Mkataba mzuri wa msaada wa udhibiti wa tabia

• Rufaa ya tathmini ya pombe/dawa

• Njia zingine zinazofaa kwa nidhamu maalum (nidhamu maalum inajumuisha uzuiliwaji, Kuondoshwa kwa muda darasani, Kuondoshwa kwa muda shuleni

# Mifano ya Hatya za Kinidhamu Zilizopendekezwa kwa Kuongezea Mbinu za Mwongozo Zilizotumika (Kiwango cha 3)

• Kusimamishwa kwenda safari za nje, mikusanyiko, au faida zingine maalum

• Kutengwa kufanya shughuli za ziada

• Faida za usafirishaji kusimamishwa

• Kutengwa kwenda hafla maalum au mazoezi ya uendelezaji

• Rufaa na mashauriano na polisi wa shule

• Kuondoshwa kwa muda shuleni (siku 4-10)

# Matendo ya Kiwango cha 4

**Matendo ya Kiwango cha 4 ni mabaya sana** na yanaweza kuwa tishio kwa afya, usalama, au mali ya mtu yeyote. msimamizi hujulishwa wakati matendo ya Kiwango cha 4 yanapotokea kwa njia ya rufaa ya nidhamu au taarifa inayoelezea tukio hilo. Wanafunzi wanaweza kusimamishwa au kufukuzwa kwa ajili ya vitendo vya kiwango cha 4. Wasimamizi wa shule wanahitajika kushauriana na Msimamizi Msaidizi wao na Ofisi ya Huduma za Usaidizi wa Wanafunzi kabla ya kuendelea na shtaka la Shambulio,Shambulio Lililochochewa, au Silaha. Vitendo vilivyoorodheshwa katika italiki husababisha arifaya lazima kwa polisi wa shule kulingana na Kanuni ya Shule Sehemu ya 1303-A (b) na 22 Pa. Kanuni Sehemu ya 10.22.

**404. Kushambulia Mfanyakazi wa Shule*: Wakati mwanafunzi anafanya vitendo vifuatavyo vyovyote dhidi ya wa shule au kontrakta (1)anajaribu kusababisha au kwa makusudi, akijua, au bila kujali kusababisha jeraha la mwili bila uchochezi wa mwili; (2) bila kujali kusababisha jeraha la mwili na silaha mbaya; au (3) majaribio ya hatari ya kimwili ya kumtia mwingine hofu ya kuumia vibaya kwa mwili.**

**405.A. Shambulio kwa Mwanafunzi au Mtu Mwingine Asiyeajiriwa na Shule*:** Wakati mwanafunzi kwa makusudi na bila uchochezi anapiga, anapiga ngumi na mateke mwanafunzi au mtu mwingine asiyeajiriwa na shule. Mwenendo mwingine wa kimwili ambao haukidhi ufafanuzi wa shambulio unaweza kuwa chini ya uzuizi dhidi ya kupigana,u chokozi/ugomvi, uonevu, unyanyasaji, na/au kuchochea usumbufu au ghasia nyingi.

**405.B Shambulio Mbaya kwa Mwanafunzi au Mtu Mwingine Asiyeajiriwa na Shule*:** Wakati mwanafunzi (1) anajaribu kusababisha jeraha kubwa la kimwili kwa mwingine, au husababisha jeraha kama hilo kwa kukusudi, akijua au bila kujali chini ya hali zinazoonyesha kutokujali sana kwa thamani ya maisha ya mwanadamu; au (2) majaribio ya kusababisha au kwa kukusudia au kwa kujua husababishajeraha la kimwili kwa mwingine na silaha mbaya.

**406. Silaha na Vifaa Hatari*: Mwanafunzi hatamiliki, kushughulikia, au kusambaza silaha akiwa kwenye mali yoyote ya** shule, katika shughuli yoyote inayodhaminiwa au kuidhinishwa na shule au wakati anatembea au anasafirishwa kwa njia yoyote kwendaaukutoka shuleni au shughuli inayodhaminiwa au kuidhinishwa na shule.

Neno "silaha," linajumuisha lakini haijakomea tu kwa kisu chochote, chombo cha kukata, zana ya kukata, kulipuzi, nunchaku, bunduki ndogo, bunduki kubwa, na/au chombo chochote, chombo au kutekeleza uwezo wakuumiza mwili. Rungu au kinyunyizi cha pilipili, ikiruhusiwa au kutishiwa kuruhusiwa, inachukuliwa kuwa silaha. Shule zitashauriana na Ofisi ya Huduma za Usaidizi wa Wanafunzi kuhusu kitu kingine chochote kinachodhaniwa kuwa zana, chombo au kinachweza kuumiza mwili kabla ya kutoa adhabu ya kinidhamu kwa ajili ya kukiuka sheria hii. Wakati wa kuamua kama kitu ni silaha, lazima shule zizingatie kitu hicho kimekusudiwa kufanya kazi. Namna ambayo mwanafunzi hutumia kitu haibadilishi silaha isiyo silaha kuwa silaha.

Silaha zinazofanana na zinazoigwa zinafafanuliwa kama vifaa vyovyote vya kuchezea au silaha ya mfano ambayo inaonekana kama silaha halisi ya kuchukuliwa kimakosa kuwa moja zao. Mwanafunzi yeyote anayewasilisha silaha inayofanana kwa mfanyakazi au mwanafunzi mwingine kama silaha halisi na/au anayetumia kutisha, kushambulia, au kunyanyasa mtu atachukuliwa kama alitumia silaha halisi, kulingana na serikali na shirikisho. (24 P.S.§ 13-1317.2). PPS ina mamlaka ya kuwaadhibu wanafunzi ambao wanatumia mfano wa silaha lakini hawahitajiki kufukuzwa kwa mwaka mmoja (1) chini ya Sheria ya 26.

Wasimamizi wa shule wanahitajika kushauriana na Msimamizi Msaidizi wao aliyechaguliwa kabla ya kuendelea na shtaka la Shambulio, Shambulio lililochochewa, au Silaha.

**407. Umiliki, Matumizi, au Kuwa Chini ya Ushawishi wa Pombe au Dawa za Kulevya:** Mwanafunzi hatamiliki, kutumia, kusambaza, au kuwa chini ya ushawishi wa kileo cha aina yoyote. Hata hivyo, katika kujaribu kupunguza nidhamu ya kutengwa,jibu nzuri la kushughulikia utunzaji wa dawa kulingana na ukali wa kosa imeainishwa kulingana na kategoria za makosa ya dawa kwenyeukurasa au kurasa zinazofuata. Hii inajumuisha kumiliki dawa zote; kiwango kubwa cha dawa zinazofikia kigezo cha kusudi la kusambaza; idadi ya bangi zaidi ya gramu 5 na makosa ya kurudia ya bangi na pombe yanayotokea katika mwaka mmoja wa shule.

Tafadhali kumbuka kuwa matumizi ya dawa kama ilivyoidhinishwa na maagizo ya matibabu kutoka kwa daktari aliyesajiliwa kwa mwanafunzi ambaye dawa imeagizwa hayatazingatiwa kama ukiukaji wa sheria hii lakini inaweza kuwa ukiukaji wa sera ya Matumizi ya Dawa. Kukosa kufuata Sera ya Matumizi ya Dawa pia kunaweza kusababisha nidhamu ya shule.

Kama sehemu ya juhudi za Wilaya kuendelea kurekebisha mchakato wa kupunguza nidhamu ya kutengwa, utaratibu uliowekwa wa jibu la kiutawala kwa ajili ya ukiukaji wa dawa za kulevya na pombe umetumika.

**Ufafanuzi unaohusiana na chati ya mwitikio ulio hapa chini uko kwenye ukurasa ufuatao.**

- **Dawa za kulevya:** Dawa yoyote ya kulevya, dawa yenye kuleta njozi, amfetamini, barbiturate, dawa nyingine ya sumu au dawa inayosababisha athari ya ulevi au kusumisha, dawa za kubuni, steroidi ya anaboli au dawa nyingine yoyote inayodhibitiwa, kama ilivyoainishwa katika Ratiba I hadi V ya Sheria ya Dawa Zinazodhibitiwa (21 USC § 812) na kufafanuliwa zaidi na kanuni katika 21 CFR Sehemu 1308.11 hadi 1308.15, au kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Dawa Inayodhibitiwa, Kifaa na Vipodozi (35 PS §780-101), Sheria ya Pennsylvania ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya na Pombe (71 PS. §1690.101), (kwa pamoja "Sheria") au kanuni zozote zinazohusiana na Sheria, au amri au kanuni zozote za mrithi.
- **Bangi:** Inahusu bangi, mafuta ya THC, au vitu vyovyote vile kwa aina yoyote, ikiwemo lakini haijakomea tu kwa, msingi wa nta, chakula, kidonge, mafuta, fomu kama jeli, mafuta au marashi, fomu zinazosimamiwa na vaporization au nebulization, tincture, au kioevu.
- **Pombe:** Kinywaji chochote chenye kileo, kinywaji cha kimea cha pombe, divai iliyoimarishwa, au kileo kingine.
- **Vifaa:** Karatasi za kuviringa, vipande vya sigara ya bangi, chombo cha kuzuia mtiririko wa damu, mabomba au sehemu za bomba, na vifaa vingine vya kutengeneza nyumbani vinavyotumika kwa kumeza dawa.
- **Mabaki ya** Dawa za Kulevya: Kiasi kidogo cha dawa kinachosalia baada ya uwepo wa dutu kubwa kutumiwa au kuondolewa (kwamfano, utomvu ambayo ni zao la bangi).
- **Kurudia Makosa ya Dawa za** Kulevya na Pombe: Kosa la pili au linalofuata la dawa ya kulevya na pombe katika wa shule. Makosa yote katika muda wa mwaka mmoja wa shule yatajumuisha makosa kutoka shule za awali ambazo mwanafunzi ameandikishwa. Wakati mwanafunzi

ana makosa zaidi ya moja ya dawa za kulevya na pombe katika mwaka mmoja wa shule, kosa lolote linalohusiana na dawa za kulevya na pombe katika mwaka unaofuata wa shule huchukuliwa kuwa kosa la kurudia.

- Programu ya ATOD: Mpango wa Kubadilisha Pombe, Tumbaku, na Dawa Zingine za Kulevya
- IAES: Mazingira ya Muda wa Elimu Mbadala

**Kategoria za Makosa ya Dawa za kulevya na Muundo wa Majibu**

Muundo ulio hapa chini wa majibu unatumika kwa wanafunzi wa elimu ya kawaida ambao hawatastahiki kupata huduma za IEP. Muundo wa majibu uliopendekezwa kwa wanafunzi wenye ulemavu ambao wanastahili IEP wanajulikana katika italiki. Wanafunzi walio na mipango ya 504 wana haki ya ulinzi sawa wa nidhamu kama ile wanafunzi wenye IEPs walipewa. Ingawa uwekaji wenye masharti wa siku 45 kwa ajili ya ukiukaji mkubwa haupatikani kiotomatiki kwa mwanafunzi aliye na Mpango wa 504, Timu ya 504 ya mwanafunzi, pamo ja na Mzazi/ Mlezi, inaweza kukubali kuwa uwekaji wa siku 45 unafaa, mradi huduma katika Mpango wa mwanafunzi 504 unaweza kutekelezwa vizuri katika mpangilio mbadala. Kwa wanafunzi walio na Mipango 504, shule zinaelekezwa kushauriana na Ofisi ya Huduma za Usaidizi wa Wanafunzi na Idara ya Sheria kupata mwongozo. Wakati ulioelezwa wa kusimamishwa kwa ajili ya ukiukaji wa Kiwango cha 3/ Kanuni ya 307 unaweza kupunguzwa baada ya kuhudhuria mpango wa kupunguza Pombe, Tumbaku, na Dawa zingine (ATOD). Hasa, mwanafunzi atatumikia siku tano (5) za kipindi cha kusimamishwa (siku mbili (2) kwa wanafunzi walio na IEPs) na siku zilizosalia zitafanyika katika muda wa kusubiri fursa ya kuhudhuria Mpango wa ATOD kama ilivyoainishwa katikamiongozo hii.

| **Makosa ya Dawa za Kulevya** Kategoria | **KIWANGO CHA 3** Kusimamishwa kwa Siku 10 Kusimamishwa kwa Siku 3 | **KIWANGO CHA 4** Kusimamishwa kwa Siku 10 + Kufukuzwa (Elimu Mbadala) Kusimamishwa kwa Siku 3 + Upangaji wa Muda wa Siku 45 Mipangilio ya Elimu Mbadala |
|---|---|---|
| **Vifaa (Kosa la Kwanza au la Kurudia)** | Umiliki wa vifaa na uwepo wa bangi (mabaki au kiwango chini ya gramu 5) | Kosa la kurudia la umiliki wa vifaa na uwepo wa bangi (kiasi chochote) |
| **Aina ya Dawa ya Kulevya: Pombe, Bangi, au Dawazingine (Kosa la kwanza au la kurudia)** | Kosa la kwanza la kupatikana na pombe; Kosa la kwanza kupatikana na bangi (mabaki au kiwango chini ya gramu 5) | Kosa la kurudia la kumiliki pombe **; Kosa la kurudia la kumiliki bangi (kiwango yoyote); Kosa la kwanza la kumiliki bangi (zaidi ya gramu 5); Umiliki wa dawa zingine isipokuwa bangi |
| **Nia ya Kusambaza** | | Kumiliki bangi zaidi ya gramu 5 |
| **Kiwango** | Umiliki wa bangi (mabaki au kiwango chini ya gramu 5) | Umiliki wa bangi zaidi ya gramu 5 au dawa nyingine yoyote au pombe |

| Safu ya Msaada | Aina ya Huduma kulingana na Kiwango cha Kosa la Kanuni za Maadili | Mpango na Mtoa Huduma*** |
|---|---|---|
| **Safu ya 3: Makosa ya Kurudia na/au Makubwa** | Marejeleo ya Uchunguzi wa SAP<br>Mbadala wa Kuondoshwa kwa muda shuleni<br>(ATOSS) Mpango<br>Madarasa na Huduma za Elimu ya Dawa za Kulevya (Kanuni za Maadili ya Ukiukaji: Kiwango cha 4) | Kituo cha Mafanikio ya Wanafunzi<br>Mpango wa ATOSS/ Uwekaji wa Elimu Mbadala Watoa Huduma wa SAP Waliochaguliwa (wanafunzi wanaweza kupata huduma za wakati mmoja wakati wa uwekaji wa elimu mbadala)<br>Makaazi ya Matibabu ya Kulazwa |
| **Safu ya 2:Makosa Madogo ya Mara ya Kwanza** | Marejeleo ya Uchunvuzi wa Mbadala wa Kuondoshwa kwa muda shuleni<br>(ATOSS) Mpango<br>(Ukiukaji wa Kanuni ya Maadili: Kiwango cha 3) | Watoa Huduma wa SAP Waliochaguliwa SHORES<br>Kituo cha Mafanikio ya Wanafunzi<br>ATOSS Mpango/Uwekaji wa Elimu Mbadala Kituo Ambacho Hujali Mpango wa ATOSS<br>Mpango wa Elimu ya Dawa za Kulevya kwa Vijana ya Three Rivers |
| **Safu ta 1: Uzuiaji Ulimwenguni** | Wasemaji wa Uhamasishaji na Elimu ya Dawa za Kulevya | Wafanyakazi wa Urejeshaji wa Allegheny CVS Inajali Uhamasishaji wa Dawa za Kulevya kwenye opioid |

### Mpango wa Pombe, Tumbaku na Dawa Zingine (ATOD)

Wilaya hutoa Mpango wa Kubadilisha Pombe, Tumbaku, na Dawa Nyingine (ATOD) kwa wanafunzi mbao wamekiuka Kanuni za Maadili ya Wanafunzi zinazohusiana na dawa za kulevya, pombe au kuvita sigara. Kwa kila mwaka wa shule, shule zote zitapokea taarifa ya tarehe na nyakati ambazo Mpango wa ATOD utakuwa na vikao vya wanafunzi na/au wazazi/walezi. Vikao hivyo vitakuwa angalau na urefu wa saa tatu (3). Lazima wanafunzi wakamilishe Vipindi viwili (2) vya Jumamosi au vipindi vitatu (3) vya jioni. Lazima Wanafunzi wamalize kozi zilizotajwa hapo juu zinazohitajika kati ya siku 60 za kosa hilo ili siku za ziada za kusimamishwa zisitumike kwa wakati huo. Lazima wanafunzi wakamilishe kila kikao (1, 2 na 3 siku za wiki na 1 na 2 siku ya Jumamosi.)

Mkuu wa shule au mhusika anayeshughulikia nidhamu ya makosa ya dawa za kulevya na pombe atampa mwanafunzi na mzazi/ mlezi nakala ya huduma za ATOD zilizosasishwa na barua ya maelezo ya misaada na Ilani ya awali ya Kusimamishwa. Barua ya huduma ATOD na maelezo ya misaada itaelezea tarehe, nyakati, na eneo la huduma na misaada yote ya ATOD.

Huduma na misaada ya ATOD pia inaweza kutumika kikamilifu kwa wanafunzi. Kwa mfano, ikiwa mwanafunzi anapatikana akiwa amelewa au ananuka bangi.

Kwa wanafunzi ambao wamefungwa kwa sababu ya makosa yao ya Kanuni za Maadili na watekelezaji wa sheria, kutengwa shuleni hakuwezi kuanza hadi mwanafunzi aachiliwe. Vivyo hivyo, ratiba ya siku 60 ya kukamilisha Mpango wa ATOD haitaanza hadi mwanafunzi atolewe kutoka jela.

### Ushirikishwaji wa Utekelezaji wa Sheria na Vitu vya Upimaji

Mwanafunzi anapopatikana na dawa za kulevya au pombe kama ilivyozuiliwa na Sera ya Bodi, Idara ya Usalama wa Shule itaarifiwa ukiukaji huo bila kuchelewa. Uhifadhi wa ushahidi unaofaa na mfululizo wa taratibu za utunzaji wa Idara

ya Usalama wa Shule utafuatwa. Idara iliyopewa ya Afisa wa Polisi wa Usalama wa Shule atakuwa na jukumu la kupakia dutu au kitu kilichokatazwa. Upimaji wa awali wa kituo wa dawa au mabaki yaliyokatazwa ni jukumu la Afisa wa Polisi wa Shule aliyechaguliwa. Dawa hiyo itapewa kwa Maabara ya Uhalifu ya Kaunti ya Allegheny kwa upimaji zaidi. Ripoti ya siri ya Matokeo ya Maabara na Ripoti ya Sehemu ya Kemia hutolewa kwa Idara ya Usalama wa Shule. Ripoti za Maabara ya Uhalifu zitatolewa kwa Ofisi ya Huduma za Usaidizi wa Wanafunzi.

Umiliki wa kalamu ya vape iliyo na mafuta ya THC ni ukiukaji wa sera ya Wilaya ya dawa na pombe. Yaliyomo kwenye kalamu za vape yatapimwa ili kubaini ikiwa dutu hii ni mafuta ya THC. Wanafunzi ambao wanamiliki kalamu mbili za vape zilizo na THC watashughulikiwa chini ya Kanuni ya 307. Umiliki wa kalam tatu (3) za vape au zaidi zenye THC watashughulikiwa chini ya Kanuni ya 407.
Kurudia ukiukaji wa kalamu ya vape pia itashughulikiwa chini ya Kanuni ya 407.

**308.** Uchomaji wa mali kwa makusudi: Kuanzisha moto au mlipuko kwa makusudi, au kusaidia, kuuliza, au kumwambia mtu mwingine, kuanzisha moto au mlipuko, ambao unaweza au unaweka mali au katika hatari ya kuharibiwa au mtu (ikiwemo mzimamoto) katika hatari ya **kuumia.**

**318. Mateso Makali:** Hutokea wakati mtu anafanya kitendo cha kudhalilisha kama ilivyoainishwa katika Kanuni ya 218 ambayo inasababisha majeraha mabaya ya kimwili au kifo kwa mwanafunzi na:

1. Mwanafunzi hufanya vitendo bila kujali afya na usalama wa mwanafunzi aliyeathiriwa; au
2. Mwanafunzi husababisha, kushurutisha au kulazimisha unywaji wa pombe au dawa ya kulevya kwa mwanafunzi aliyeathiriwa.

*Wasimamizi wa shule wanashauriwa kushauriana na Ofisi ya Huduma za Usaidizi wa Wanafunzi kabla ya kumshutumu mwanafunzi kwa ukiukaji wa Shambulio au Silaha.

# Mifano ya Uingiliaji wa Mwongozo/ Mwendelezo wa Mbinu (Kiwango cha 2)

• Matumizi ya Kanuni za Urekebishaji (k.v taarifa nzuri, maswali ya urejesho, vikundi, mikutano midogo isiyopangwa, mkutano rasmi wa urejesho, n.k.)

•Rufaa kwa Mchakato wa Mifumo Mingi ya Msaada(MTSS)

•Rufaa kwa mipango ya utatuzi wa mizozo shuleni (kwa mfano, upatanishi wa wanarika)

• Mkutano wa Mwanafunzi/Mwalimu

• Mkutano wa Mzazi au Mlezi/Mwalimu

• Mkutano wa Mwanafunzi/Msimamizi

• Uingiliaji kati wa kushauri wafanyakazi/mkutano wa mwongozo

• Kazi ya kutafakari iliyoandikwa

Unda, kagua, au rekebisha vifaa vya kupanga mwanafunzi (k.m., Mpango wa Kusaidia Tabia)

• Badilisha katika ratiba au darasa (na arifu ya mzazi/mlezi)

• Ushauri wa Mtu Binafsi/Kikundi

Rufaa kwa Mpango wa Usaidizi wa Wanafunzi (SAP) kwa ajili ya uzuizi (k.m. vikundi vya mafundisho ya ustadi wa kijamii na kihisia kama udhibiti wa hasira, mbadala wa uchokozi, ustadi wa kupanga) na/au huduma za uingiliaji (k.v. huduma za ushauri wa afya ya kitabia)

• Mpango wa tabia ya mwanafunzi

• Rufaa kwa mpango wa ushauri

• Rufaa kwa Shirika la Jumuiya Lililoidhinishwa na Wilaya (CBO)

• Huduma ya jamii (kwa idhini ya mzazi/mlezi)

• Mkataba mzuri wa msaada wa udhibiti wa tabia

• Rufaa ya tathmini ya pombe/dawa

• Njia nyingine zinazofaa za nidhamu maalum (nidhamu maalum inajumuisha uzuiliwaji, Kuondoshwa kwa muda darasani, Kuondoshwa kwa muda shuleni)

# Mifano ya Hatua za Kinidhamu Zilizopendekezwa kwa Kuongezea kwa Mbinu za Mwongozo Zilizotumika (Kiwango cha 3)

• Kusimamishwa kwenda safari za nje, mikusanyiko, au faida zingine maalum

• Kutengwa kufanya shughuli za ziada

• Faida za usafirishaji kusimamishwa

• Kutengwa kwenda hafla maalum au mazoezi ya uendelezaji

• Rufaa na mashauriano na polisi wa shule

• Kuondoshwa kwa muda shuleni

• Kutengwa/kufukuzwa (siku 11 au zaidi)

• Mpango mbadala wa elimu